# *GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR*

***(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)***

**Sehemu ya CXXXII Nam. 7174** **07 Novemba , 2023** **Bei Shs.4,000/=**

*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti* *Hutolewa kila Ijumaa*

**YALIYOMO**

*Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar, Nam. 12 ya 2019 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar Kusimamia Huduma za Serikali Mtandao Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo .................................... 933

**SEHEMU YA SHERIA**

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

**Tangazo la Mswada**

Nam. :- Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar

**TANGAZO**

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanzia tarehe 29 Novemba, 2023 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

**ZANZIBAR**
07 Novemba, 2023

(Mhandisi. Zena Ahmed Said)
***Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.***

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

**MSWADA**

*wa*

**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA WAKALA WA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR, NAM. 12 YA 2019 NA KUTUNGA SHERIA YA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR KUSIMAMIA HUDUMA ZA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar, 2023 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais.

Matumizi.

**2.** Sheria hii itatumika kwa taasisi zote za umma na watumishi wa umma katika masuala yanayohusiana na matumizi na vifaa vya TEHAMA katika huduma za Serikali mtandao Zanzibar.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka iliyoanzishwa chini ya masharti ya kifungu cha 8 cha Sheria hii;

"data" maana yake ni taarifa yoyote iliyotolewa kwa njia ya kielektroniki;

"huduma ya Serikali mtandao" maana yake ni huduma yoyote ya umma inayotolewa kwa njia ya kielektroniki na taasisi yoyote ya umma;

"kumbukumbu ya kielektroniki" maana yake ni kumbukumbu iliyotengenezwa, iliyoanzishwa, iliyotumwa, iliyowasilishwa, iliyopokelewa, iliyohifadhiwa au iliyopatikana kwa njia ya kielektroniki;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar iliyoanzishwa chini ya masharti ya kifungu cha 4(1) cha Sheria hii;

"mawasiliano ya kielektroniki" maana yake ni uhamishaji wowote wa alama, ishara au data za kompyuta za aina yoyote zinazosambazwa kwa ukamilifu au sehemu yake kwa kutumia waya, redio, mionzi ya kieletroniki, picha ya kielektroniki, miwani ya picha au kwa muundo mwengine wowote unaofanana na huo;

"Mdhibiti wa Data" maana yake ni mtu, kampuni au chombo chengine ambacho kinaamua madhumuni na njia za kuchakata data binafsi;

"Mfumo wa taarifa" maana yake ni mfumo wa kuzalisha, kutuma, kupokea, kuhifadhi, kuonyesha au vyenginevyo kuchakata ujumbe wa data;

"Mfumo wa TEHAMA" maana yake ni mfumo wowote wa TEHAMA unaojumuisha vifaa vya kompyuta, programu za kompyuta, data, teknolojia ya mawasiliano na watu ambao wanaozitumia;

"miundombinu" maana yake ni nyenzo na mifumo ya lazima inayowezesha taasisi za umma, biashara na jamii kwa ujumla kupata huduma za Serikali mtandao;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 14(1) cha Sheria hii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

"Serikali mtandao" maana yake ni matumizi ya TEHAMA katika utendaji wa Serikali na utoaji wa huduma za umma;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)" maana yake ni TEHAMA inayojumuisha nyenzo na rasilimali za teknolojia zinazotumika kubuni, kuchakata, kuhifadhi, kuwasiliana, kusambaza na kupata taarifa katika utumishi wa umma;

"Usalama wa TEHAMA" maana yake ni kulinda mfumo wa taarifa dhidi ya upatikanaji, utumiaji, utoaji, uingiliaji, urekebishaji au uharibifu usioruhusiwa kwa madhumuni ya kuweka usiri, uadilifu na upatikanaji wa mfumo wa taarifa;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na Serikali mtandao.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHWAJI WA MAMLAKA

Kuanzishwa kwa Mamlaka.

**4.-**(1) Kunaanzishwa Mamlaka itakayojulikana kama Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar na ufupisho wake utakuwa ni eGAZ.

(2) Mamlaka itakuwa ni chombo kinachojitegemea chenye urithi wa kuendelea, chenye muhuri na kwa jina lake, kwa mujibu wa sheria, kitakuwa na uwezo wa:

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kupata, kumiliki, kununua na kuondosha mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika;

(c) kuingia katika mikataba au miamala yoyote;

(d) kukopa au kukopesha kiasi chochote cha fedha kutoka taasisi yoyote ya fedha; na

(e) kutekeleza au kufanya kitendo au jambo jengine lolote ambalo kisheria linaweza kutekelezwa au kufanywa na chombo kinachojitegemea.

Muhuri na nembo ya Mamlaka.

**5.-**(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Mamlaka katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Mamlaka katika waraka wowote yatathibitishwa na saini ya Mkurugenzi Mkuu au afisa mwengine yeyote wa Mamlaka aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Mamlaka utawekwa muhuri wa Mamlaka na utathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Kazi za Mamlaka.

**6.** Mamlaka itakuwa na kazi za:

(a) kupanga, kuratibu, kufuatilia na kusimamia huduma zote za Serikali mtandao, viwango na kutoa miongozo katika taasisi za umma;

(b) kutoa na kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za Serikali mtandao katika njia tofauti;

(c) kuzisimamia taasisi za umma katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA, sheria, kanuni, viwango na miongozo inayohusiana na Serikali Mtandao;

(d) kutoa ushauri au msaada wa kitaalamu kuhusiana na masuala ya Serikali mtandao katika taasisi za umma;

(e) kuanzisha na kutunza kumbukumbu za wataalamu wa TEHAMA na kuratibu matumizi ya wataalamu hao katika utumishi wa umma na kuwaendeleza kwa mafunzo endelevu;

(f) kuthibitisha mifumo ya taarifa inayoendana na mahitaji ya ulinzi na usalama;

(g) kuthibitisha mifumo na vifaa vya TEHAMA ambavyo vitatumika katika taasisi za umma;

(h) kuendeleza miundombinu ya pamoja wezeshi ili kuhakikisha upatikanaji sawa wa huduma za Serikali mtandao;

(i) kuweka vigezo na viwango vya ununuzi wa programu na vifaa vya TEHAMA vinavyohusiana na huduma za Serikali mtandao katika taasisi za Umma;

(j) kutathmini huduma za Serikali mtandao katika taasisi za umma;

(k) kutoa maelekezo kwa taasisi za umma katika utekelezaji wa sera za Serikali mtandao;

(l) kuzisimamia taasisi binafsi zinazofanya kazi zozote zinazohusiana na Serikali mtandao kwa niaba ya Serikali;

(m) kukuza na kufanya utafiti na uvumbuzi kuhusiana na masuala ya Serikali mtandao katika taasisi za umma na kutoa mapendekezo kwa Serikali; na

(n) kutekeleza kazi nyengine yoyote ambayo inaweza kuwa muhimu kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

Uwezo wa Mamlaka.

**7.** Mamlaka, katika kutekeleza kazi zake chini ya masharti ya Sheria hii, itakuwa na uwezo wa:

(a) kuitaka taasisi ya umma kutoa taarifa, nyaraka, kumbukumbu au ripoti kuhusiana na TEHAMA katika utengenezaji na uanzishwaji wa mifumo, miundombinu na miradi ya huduma za Serikali mtandao;

(b) kuidhinisha mikakati ya kisekta ya maendeleo ya Serikali ya kielektroniki na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya Serikali mtandao;

(c) kusimamisha utekelezaji wa miradi yoyote ya TEHAMA inayotekelezwa na taasisi za umma ikiwa haijakidhi viwango na miongozo ya Serikali Mtandao na viwango vya kimataifa;

(d) kutoa maelekezo kwa utekelezaji wowote wa sera za Serikali mtandao na miradi ya TEHAMA inayofanywa na taasisi za umma ambao hauzingatii viwango na miongozo ya Serikali mtandao;

(e) kupata msaada wa kitaalamu au kiufundi kutoka taasisi yoyote inayofaa ya ndani au nje ya Zanzibar;

(f) kuingia katika mahusiano na taasisi nyengine za kitaifa au kimataifa kwa manufaa ya Mamlaka na nchi;

(g) kufikia mfumo wa TEHAMA, miundombinu au mitandao kwa taasisi yoyote ya umma kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi wa TEHAMA au tathmini ya usalama wa TEHAMA inayohusiana na huduma za Serikali mtandao;

(h) kusimamia malalamiko yanayohusiana na huduma za Serikali mtandao kutoka kwa umma, watoa huduma au mtu yeyote; na

(i) kutoza ada, tozo au malipo mengine kwa mtu au taasisi yoyote kutokana na huduma inazozitoa.

## SEHEMU YA TATU
## UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA MAMLAKA

Uanzishaji na Muundo wa Bodi.

**8.** Kutakuwa na Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mkuu;

(c) Katibu Mkuu kutoka Wizara inayohusika na Fedha au mwakilishi wake;

(d) Katibu Mkuu kutoka Wizara inayohusika na TEHAMA au mwakilishi wake;

(e) Katibu Mkuu kutoka Wizara inayohusika na Serikali mtandao au mwakilishi wake;

(f) Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano la Zanzibar; na

(g) Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu ambaye atateuliwa na Waziri baada ya kushauriana na Mwanasheria Mkuu.

Sifa za Mwenyekiti.

**9.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya TEHAMA, Sayansi ya Kompyuta, Uhandisi, Uchumi, Fedha, Utawala, Biashara, Sheria au fani nyengine yoyote inayolingana nazo kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(c) ana uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba na kiwango cha juu cha uweledi wa kusimamia kwa ufanisi masuala ya taasisi za umma au binafsi; na

(d) ana uadilifu wa hali ya juu.

Katibu wa Bodi.

**10.-**(1) Bodi itamteua mfanyakazi wa Mamlaka kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Mfanyakazi wa Mamlaka atakuwa na sifa ya kuwa Katibu wa Bodi ikiwa :

(a) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria au ana sifa ya kuwa katibu wa shirika kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali; na

(b) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano katika utumishi wa umma.

(3) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi na atakuwa na:

(a) ataandaa ajenda za vikao vya Bodi kwa kushauriana na Mwenyekiti;

(b) atachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(c) atatunza taarifa sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(d) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa wajumbe;

(e) atatoa ushauri kwa Bodi pale utakapohitajika; na

(f) atafanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Bodi kwa mujibu wa sheria.

Kazi za Bodi.

**11.** Kazi za Bodi zitakuwa ni:

(a) kusimamia na kufuatilia sera ya Serikali mtandao na kupendekeza mapitio ya sera hiyo;

(b) kusimamia kazi za Mamlaka chini ya masharti ya Sheria hii;

(c) kuishauri Serikali kuhusu masuala yote yanayohusiana na Serikali mtandao;

(d) kupitia na kuidhinisha mipango ya biashara na uendeshaji, bajeti, ripoti na ukaguzi wa taarifa za fedha za Mamlaka;

(e) kupitia na kuidhinisha ripoti ya ukaguzi ya mfumo wa kitaalamu; na

(f) kufanya kazi nyengine yoyote iliyotolewa chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote ambayo inaweza kuwa muhimu kwa ajili ya kufikia malengo ya uanzishwaji wa Mamlaka.

Uwezo wa Bodi.

**12.** Bodi, katika kutekeleza kazi zake, itakuwa na uwezo wa:

(a) kumuelekeza Mkurugenzi Mkuu kuwasilisha taarifa yoyote, ripoti au nyaraka nyengine ambazo Bodi itaona ni muhimu;

(b) kutoa maelekezo halali kwa Mkurugenzi Mkuu kuhusiana na uendeshaji na utekelezaji wa Mamlaka;

(c) kuidhinisha:

(i) mipango kazi na malengo ya idara na vitengo vyote pamoja na kusimamia maendeleo yao katika kuyafikia kwa utaratibu endelevu;

(ii) bajeti ya mwaka ya Mamlaka;

(iii) kanuni za fedha, kanuni za utumishi na mpango kazi wa Mamlaka;

(d) kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011, kuweka vigezo na masharti ya utumishi, mishahara na maposho ikijumuisha stahiki nyengine zozote kwa wafanyakazi wa Mamlaka;

(e) kupendekeza muundo wa utumishi wa Mamlaka kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011;

(f) kusimamia maadili ya kazi, nidhamu na viwango vya kitaalamu kwa waajiriwa wa Mamlaka;

(g) kusikiliza rufaa na kuchukua hatua stahiki za kuwarekebisha waajiriwa wa Mamlaka kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011, kanuni za wafanyakazi na kanuni za maadili;

(h) kuajiri na kuwapandisha vyeo wafanyakazi wa Mamlaka kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011;

(i) kutoa miongozo mbalimbali kwa waajiriwa wa Mamlaka kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa Mamlaka;

(j) kuidhinisha ada na tozo kwa huduma zinazotolewa na Mamlaka; na

(k) kuidhinisha malengo, shabaha na vipimo vya utendaji wa Mamlaka.

Mwenendo wa Bodi.

**13.** Masharti yanayohusiana na mwenendo wa Bodi yatakuwa kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Sheria hii.

Uteuzi na sifa za Mkurugenzi Mkuu.

**14.-**(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya Sayansi ya Kompyuta, Teknolojia ya Habari, Uhandisi wa Mawasiliano ya Simu, Mawasiliano ya Data au fani nyengine yoyote inayolingana na hizo kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(c) ana uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba katika fani zinazohusika; na

(d) ana uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

**15.-**(1) Mkurugenzi Mkuu atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka na atawajibika kwa utekelezaji wa kazi za kila siku za Mamlaka.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu:

(a) atasimamia mali na shughuli za Mamlaka;

(b) ataisimamia Mamlaka ili kuhakikisha kuwa malengo ya uanzishwaji wa Mamlaka yanafikiwa;

(c) atapendekeza na kutekeleza mpango mkakati wa biashara na uendeshaji wa Mamlaka; na

(d) atafanya kazi nyengine yoyote kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii kama atakavyopangiwa na Bodi.

Idara, vitengo na divisheni.

**16.-**(1) Mamlaka itaanzisha idara, vitengo na divisheni kama itakavyoamuliwa na Bodi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

(2) Wakurugenzi wa Idara watateuliwa na Bodi kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(3) Mameneja wa vitengo na wakuu wa divisheni watateuliwa na Mkurugenzi Mkuu kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(4) Wakurugenzi, Mameneja na wakuu wa divisheni watawajibika kwa Mkurugenzi Mkuu.

Wafanyakazi wa Mamlaka.

**17.-**(1) Kutakuwa na wafanyakazi wa Mamlaka ambao wataajiriwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

(2) Mamlaka inaweza kuteuwa watendaji wengine wa TEHAMA katika taasisi za umma watakaofanyakazi kwa niaba ya Mamlaka kama itakavyoelekezwa katika Kanuni.

## SEHEMU YA NNE
## MIFUMO NA HUDUMA ZA SERIKALI MTANDAO

Misingi mikuu ya Serikali mtandao.

**18.** Misingi mikuu ya Serikali mtandao:

(a) itazingatia mahitaji ya wananchi na biashara katika utoaji wa huduma za umma;

(b) itaendeleza na itatumia ubunifu na hatua ya mageuzi jumuishi ya utendaji kazi ambazo zimeratibiwa, shirikishi na zinazolenga kuwanufaisha wananchi kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma;

(c) itabuni suluhisho ili kupunguza gharama za uendeshaji za muda mrefu na kubuni fursa za kutathmini na kuondoa hatua zisizo za lazima na kupunguza mzunguko unaohusiana na taratibu za kawaida;

(d) itatumia njia ya ubadilishanaji wa taarifa za kiutendaji miongoni mwa taasisi za umma ambazo zitaepusha taarifa kujirejea;

(e) itahifadhi taarifa zilizo chini ya Mdhibiti wa Data zinazotumiwa kwa mujibu wa sheria;

(f) itatumia rasilimali za umma kwa uaminifu na uwajibikaji katika utekelezaji wa shughuli za Serikali mtandao; na

(g) itashirikiana na sekta binafsi kwa ajili ya kukuza na kuboresha matumizi endelevu ya rasilimali kutoka kwa taasisi za umma.

Kumbuku-mbu za kie-lektroniki.

**19.-**(1) Endapo sheria yoyote inaeleza kwamba kumbukumbu zihifadhiwe kwa muda wowote maalumu, sharti hilo litachukuliwa kuwa limetimizwa, ikiwa kumbukumbu hizo zimehifadhiwa katika mfumo wa kielektroniki na:

(a) taarifa iliyomo katika kumbukumbu hiyo inaweza kufikiwa ili iweze kutumika kwa marejeo yanayofuata;

(b) kumbukumbu za kielektroniki zitahifadhiwa katika mfumo unaowakilisha usahihi wa taarifa iliyotolewa, iliyotumwa au iliyopokelewa; na

(c) maelezo yanayowezesha utambuzi wa asili, sehemu, tarehe na muda wa kutuma au kupokea kumbukumbu hizo za kielektroniki yanapatikana katika kumbukumbu ya kielektroniki.

(2) Usimamizi na utumiaji wa kumbukumbu za kielektroniki za umma utafanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar, Nam. 3 ya 2008.

Malipo ya kielektro-niki na utoaji wa risiti.

**20.-**(1) Endapo sheria inahitaji malipo yoyote kufanywa katika utaratibu maalumu, sharti hilo la sheria litachukuliwa kuwa limetimizwa ikiwa malipo hayo yamefanywa kwa njia ya kielektroniki na yamezingatia masharti yote yaliyowekwa na Mamlaka.

(2) Endapo sheria inahitaji utoaji wa risiti ya malipo, sharti hilo litachukuliwa kuwa limetimizwa ikiwa risiti ipo katika muundo wa kielektroniki na inafikika na kueleweka ili iweze kutumika kwa marejeo yanayofuata.

(3) Mfumo wa uchakataji taarifa unaotumika kwa ajili ya viwango vinavyohusiana na miamala ya kielektroniki utakuwa na ulinzi wa kutosha kwa mujibu wa viwango vya teknolojia vinavyokubalika katika muda unaohusiana na uthibitishaji, uadilifu, upatikanaji na usiri wa kuchakata miamala ya kielektroniki ikijumuisha benki ya kielektroniki, benki ya simu, uhamishaji fedha za kielektroniki, sehemu ya mauzo, mashine za kutoa pesa kiotomatiki na miamala mengine inayohusiana nayo ya kielektroniki au mifumo kama itakavyoainishwa katika Kanuni.

(4) Taasisi ya umma inayojihusisha na malipo, mikataba na utoaji wa huduma za kielektroniki itakidhi mahitaji ya usalama kwa kuzingatia viwango vya tasnia husika vya teknolojia vinavyotolewa na taasisi hiyo kwa malipo ya kielektroniki au kama itakavyoainishwa katika Kanuni.

**21.** Endapo tozo au kiwango chengine kinachopokelewa kutokana na taratibu za kiutawala zilizofanywa kwa njia ya kielektroniki, Mamlaka itawezesha malipo ya tozo hizo au kiwango chengine kinachopokelewa kwa kushiriki katika angalau utaratibu mmoja unaojitosheleza wa malipo ya uhakika ambao ni wa kawaida katika eneo la muamala wa biashara ya kielektroniki.

Njia za malipo ya kielektroniki.

**22.** Kwa madhumuni ya Sheria hii, taarifa ya kielektroniki itakuwa halali au itakubalika kwa sababu kwamba, taarifa hiyo:

Uhalali wa taarifa za kielektroniki.

(a) imebuniwa, imehifadhiwa au imewasilishwa kielektroniki; au

(b) inarejewa lakini haimo katika hati ya kielektroniki, ikiwa taarifa inayorejewa inajulikana na kukubaliwa na mhusika ambaye inamuhusu.

**23.-**(1) Taasisi ya umma, endapo kutakuwa na haki ya kupatikana majalada, itatoa ruhusa ya kupatikana majalada kwa:

Upatikanaji wa majalada.

(a) kutoa nyaraka zilizochapishwa zinazohusika;

(b) kuonyesha nyaraka za elektroniki katika skrini;

(c) kusambaza nyaraka za kielektroniki za TEHAMA; au

(d) kuruhusu upatikanaji wa kielektroniki kwa maudhui yaliyomo kwenye majalada.

(2) Kila taasisi ya umma italazimika kufungua sehemu ya upatikanaji kwa ajili ya uhamishaji wa nyaraka za kielektroniki, ikijumuisha nyaraka ambazo zinatolewa zikiwa na saini ya kielektroniki inayokubalika.

**24.-**(1) Taasisi ya Umma, kabla ya uanzisha mpango wa huduma yoyote ya Serikali mtandao itatumia mbinu zilizowekwa na Mamlaka katika nyaraka, uchambuzi na uimarishaji wa taratibu za kiutawala zinazowekwa kwa mujibu wa Sheria hii.

Uimarishaji wa taratibu za kiutawala.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki “Mpango wa huduma za Serikali mtandao” maana yake ni shughuli yoyote inayofanywa na taasisi za umma kwa madhumuni ya kutekeleza sera za Serikali mtandao.

**25.-**(1) Endapo taasisi ya umma itaweka wazi upatikanaji wa mtandao kwa ajili ya kupata data, taasisi ya umma hiyo itatumia mfumo wa kusoma mashine kama msingi mkuu.

Masharti yanayohusiana na utoaji wa taarifa.

(2) Mfumo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itajumuisha data ambayo inaweza kusomwa na kuchakatwa katika hali ya kiotomatiki kwa njia ya programu inayolingana.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, data iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatolewa kwa mujibu wa chanzo cha data hiyo.

(4) Mamlaka inaweza kutoa miongozo ya matumizi ya data zilizo chini ya kifungu hiki ikijumuisha matumizi ya kibiashara na yasiyokuwa ya kibiashara, masharti ya matumizi na kutenganisha kwa dhima na dhamana.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "chanzo cha taarifa" maana yake ni mkusanyiko wa data ambayo zinatoa taarifa kuhusu data nyengine.

Masharti ya utoaji wa taarifa kwa maandishi.

**26.-**(1) Endapo sheria yoyote inahitaji au inakusudia utoaji wa taarifa kwa maandishi, taarifa ambayo imetolewa kwa njia ya kielektroniki itachukuliwa kwamba imetolewa kwa maandishi iwapo:

(a) wakati taarifa ilipotolewa, ilikuwa kawaida kutarajia kwamba taarifa ingeweza kuwa tayari kupatikana, na inaweza kuhifadhiwa kwa ajili ya rejea ya baadae za anayepelekewa;

(b) endapo taarifa hiyo itatolewa kwa Serikali na Serikali inaihitaji kwamba:

(i) taarifa itolewe kwa njia maalumu kulingana na mahitaji ya maalumu ya teknolojia; au

(ii) kitendo hicho maalumu kifanywe kwa ajili ya kuhakiki upokeaji wa taarifa hizo kukidhi mahitaji ya Serikali; na

(c) endapo taarifa hiyo itatolewa kwa mtu asiyekuwa Serikali, mtu huyo ataridhia taarifa hiyo kutolewa kwa njia ya kielektroniki.

(2) Kifungu hiki kinatumika kwa masharti au ruhusa ya utoaji wa taarifa, ikiwa litatumika au halitatumika neno lolote kati ya "kutoa", "kutuma", "kupeleka" au neno jengine lolote litalotumika kumaanisha masharti au ruhusa.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "utoaji wa taarifa" inajumuisha:

(a) ufanyaji wa maombi;

(b) ufanyaji au utumaji wa lalamiko;

(c) utoaji wa indhari;

(d) utumaji wa ritani;

(e) ubadilishaji wa ombi;

(f) utoaji wa tamko;

(g) utumaji au utoaji wa cheti;

(h) uwekaji wa pingamizi; na

(i) utoaji maelezo ya sababu.

(4) Endapo sheria chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki itahitaji zaidi ya nakala moja ya taarifa kuwasilishwa kwa mtu, sharti hilo litachukuliwa kuwa limetimizwa kwa kutoa taarifa kwa mtu huyo kwa njia ya kielektroniki kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Kubadilishana data.

**27.-**(1) Kwa madhumuni ya kuwezesha ubadilishaji wa data katika utumishi wa umma, Mamlaka itaanzisha na kusimamia jukwaa la kubadilishana data.

(2) Bila ya kuathiri sheria yoyote na kwa madhumini ya kuleta ufanisi, taasisi ya umma inaweza, katika utoaji wa huduma za Serikali mtandao, kubadilishana data kwa njia ya kielektroniki katika itakavyoainishwa na Waziri.

(3) Upatikanaji wa taarifa utakuwa kwa mujibu wa haki za mtumiaji na ngazi za upatikanaji kama itakavyoainishwa na Mamlaka katika miongozo.

Ujazaji wa nyaraka kielektroniki, saini ya kielektroniki na utoaji wa nyaraka.

**28.-**(1) Taasisi ya umma ambayo, kwa mujibu wa Sheria hii au sheria nyengine yoyote, inakubali ujazaji wa nyaraka au inahitaji nyaraka ziandaliwe, ziandikwe au zihifadhiwe, inatoa kibali, leseni au inaweka utaratibu wa ulipaji, inaweza;

(a) kukubali kujaza nyaraka kwa njia ya kielektroniki;

(b) kutoa kibali, leseni au ruhusa kwa njia ya kielektroniki;

(c) kufanya au kupokea malipo kwa njia ya kielektroniki; au

(d) kukubali kujaza nyaraka au kufanya na kupokea malipo kwa njia ya Msimbo wa majibu ya haraka “QR Code” na Msimbo Upau “Barcode”.

(2) Mamlaka inaweza, kuhusiana na taasisi ya umma inayotekeleza majukumu yake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kuainisha:

(a) namna na muundo ambao mawasiliano ya kielektroniki yatawasilishwa, yatafanywa, yatahifadhiwa au kutolewa;

(b) aina ya saini ya kieletroniki inayohitajika iwapo mawasiliano ya kielektroniki yanahitajika kusainiwa;

(c) namna na muundo ambao saini ya kielektroniki inaweza kuwekwa na kuhusishwa na mawasiliano ya kielektroniki;

(d) hatua na taratibu bora za udhibiti ili kuhakikisha uadilifu, usalama na usiri wa kutosha wa mawasiliano ya kielektroniki au malipo; na

(e) masharti mengine yoyote ya mawasiliano ya kielektroniki au malipo.

(3) Taasisi ya umma inaweza kutumia taratibu za uthibitishaji za ziada ikujumisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya uthibitishaji au vyeti vya uthibitishaji kwenye nakala zilizochapishwa au nakala

ngumu za nyaraka za kielektroniki au ujumbe wa data za kielektroniki na wathibitishaji wa kielektroniki, watoa huduma na mamlaka nyengine zinazotambulika au zilizoteleuliwa.

Kizuizi cha matumizi ya data binafsi.

**29.** Bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, taasisi ya umma itahakikisha kwamba data binafsi:

(a) inahifadhiwa na kutumika kwa madhumuni yaliyoainishwa na halali ambayo data inakusanywa na kuchakatwa; na

(b) haitowekwa zaidi ya muda unayohitajika kwa madhumuni ambayo data inakusanywa na kuchakatwa au kama itakavyotakiwa na sheria.

Kutotoa taarifa zilizopewa taasisi za umma.

**30.-**(1) Mtu, bila ya ruhusa halali, hatotoa taarifa iliyotolewa kwa Taasisi ya Umma kwa madhumuni huduma za Serikali mtandao au wakati wa utoaji wa huduma za Serikali mtandao.

(2) Mtu ambaye anakiuka masharti ya kifungu hiki, ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili.

Ulinzi wa data.

**31.** Taasisi ya umma itatekeleza na kusimamia hatua za ulinzi wa data kwa mujibu wa utaratibu utakaoainishwa katika Kanuni.

Utambulisho na uthibitisho.

**32.-**(1) Mdhibiti wa Data anaweza kutoa haki ya upatikanaji wa data binafsi ambazo kuna maslahi yanayolindwa ya usiri katika mazingira ya mawasiliano ya kielektroniki katika sekta ya umma, ambapo utambulisho wa kipekee wa mtu anayetaka kuzipata na uthibitisho wa ombi la mtu huyo umethibitishwa.

(2) Uthibitishaji chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utatolewa katika njia ambayo inaweza kuhakikiwa kielektroniki kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(3) Mdhibiti wa Data, endapo utambulisho utahitaji kuhakikiwa unaweza kuthibitishwa, atatoa ruhusa iwapo tu unahusiana na data binafsi ambapo mtu anayeziomba kupata data hizo atakuwa anapatikana kwa kutumia utambulisho huo.

(4) Utambulisho wa mtu unaweza kuombwa kwa kufanya mawasiliano na Mdhibiti wa Data na chombo cha umma, endapo itakuwa ni hitaji muhimu kwa utekelezaji wa kazi aliyopewa na Mdhibiti wa Data huyo chini ya sheria yoyote.

Masharti ya saini ya kielektroniki.

**33.-**(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, endapo sheria inahitaji saini ya mtu inayohusiana na taarifa yoyote, itachukuliwa kwamba imekidhi iwapo taarifa hiyo itatolewa kwa njia ya kielektroniki na:

(a) njia itakayotumika kumtambua mtu huyo na kuonyesha idhini ya mtu huyo kwa taarifa iliyotolewa;

(b) kwa kuzingatia mazingira yote husika, iwapo njia hiyo ilitumika, ikijumuisha makubaliano mengine yoyote husika, njia hiyo ilikuwa inakubalika na inafaa kwa madhumuni ambayo taarifa hiyo iliwasilishwa;

(c) ikiwa saini itahitajika katika taasisi ya umma na taasisi hiyo ya umma itahitaji kwamba, njia iliyotumika iwe kwa mujibu wa masharti maalumu ya teknolojia ya habari, taasisi hiyo ya umma imekidhi masharti; na

(d) ikiwa utiaji wa saini utahitajika kwa mtu ambaye si taasisi ya umma, mtu huyo akaridhia kwamba masharti yamefuatwa kwa kutumia njia iliyoainishwa katika aya (a) ya kifungu hiki.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1)(a) na (b) cha kifungu hiki, saini iliyofumbwa itachukuliwa kuwa imekidhi vigezo ikiwa saini hiyo:

(a) imeunganishwa kipekee na mtu ambaye saini yake inahitajika;

(b) ina uwezo wa kumtambua mtu huyo;

(c) imetengenezwa kwa kutumia njia ambayo mtu huyo anaweza kuidhibiti yeye mwenyewe; na

(d) imeunganishwa na taarifa ambazo zinahusiana nayo kwa namna ambayo na marekebisho yoyote ya baadaye ya taarifa yatajulikana.

## SEHEMU YA TANO
## USIMAMIZI WA HUDUMA ZA SERIKALI MTANDAO

Njia za Mawasiliano ya Kimtandao.

**34.-**(1) Mamlaka, kwa madhumuni ya Sheria hii, itatoa miongozo ya Njia za Mawasiliano ya Kimtandao ikiainisha:

(a) uhifadhi na matumizi ya barua pepe za Serikali;

(b) tovuti;

(c) mtandao wa kijamii; na

(d) majukwaa ya mawasiliano ya mtandaoni.

(2) Mamlaka itahakikisha njia za mawasiliano zinazohusiana na huduma za Serikali mtandao zinalindwa.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "Njia za Mawasiliano ya Kimtandao" maana yake ni chombo chochote cha mawasiliano ambacho taasisi ya umma au mtu anaweza kutuma au kupokea ujumbe kwa madhumuni ya Serikali mtandao.

Kutunza siri.

**35.** Mtu, bila ya ruhusa halali, hatotoa nyaraka yoyote ya Serikali, data iliyohifadhiwa kwenye kompyuta au taarifa nyengine yoyote iliyopatikana

au vyenginevyo imepatikana wakati wa utekelezaji wa kazi au uwezo wa Mamlaka chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote.

Mfumo ya TEHAMA.

**36.-**(1) Mamlaka itaanzisha, kuendeleza au kupeleka mfumo jumuishi ya TEHAMA kwa taasisi za umma yenyewe au kwa ombi kutoka taasisi ya umma husika.

(2) Maombi ya ruhusa yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, yatajumuisha masharti kama yalivyoainishwa na miongozo itakayotolewa na Mamlaka.

(3) Mamlaka itatoa mapendekezo yake kwa taasisi ya umma si zaidi ya siku kumi na nne za kazi kutoka tarehe iliyopokea ombi hilo.

(4) Bila ya kuathiri masharti chini ya Sheria hii, taasisi ya umma itakuwa na wajibu wa kutumia, kuendeleza na kutunza mfumo wake wa TEHAMA.

Ununuzi wa vifaa na programu ya TEHEMA.

**37.** Taasisi ya umma yoyote ambayo inahitaji kununua vifaa au programu ya TEHAMA kwa ajili ya utoaji wa huduma za Serikali mtandao, itafuata viwango na taratibu kama zitakavyoainishwa na Mamlaka katika miongozo.

## SEHEMU YA SITA
## USALAMA WA MFUMO WA TAARIFA NA MIAMALA YA KIELEKTRONIKI

Kuanzishwa kwa Kituo cha Operesheni ya Usalama cha Serikali mtandao.

**38.-**(1) Kutakuwa na Kituo cha Operesheni ya Usalama cha Serikali mtandao kwa ajili ya ufuatiliaji wa taarifa.

(2) Uendeshaji wa Kituo cha Operesheni ya Usalama cha Serikali mtandao utakuwa chini ya usimamizi wa Mkurugenzi Mkuu.

Usalama wa Taarifa.

**39.** Taasisi ya umma, kwa mujibu wa viwango vya usalama wa taarifa vilivyowekwa na Mamlaka:

(a) itaendeleza na kuchukua hatua za kiusalama ili kulinda taarifa zinazokusanywa au zinazotumika zinazohusiana na huduma za Serikali mtandao dhidi ya utoaji wa taarifa usioruhusiwa; na

(b) itachukua hatua stahiki ili kuhakikisha kwamba, kila afisa wa taasisi ya umma anayehusika na utoaji wa huduma au ukusanyaji, uwekaji, uingizaji au usambazaji wa taarifa au huduma anatambua na kuzingatia hatua za kiusalama zinazohusiana na usimamizi na ulinzi wa taarifa.

Ukaguzi wa mfumo wa Serikali mtandao.

**40.-**(1) Mamlaka inaweza kufanya tathmini na ukaguzi wa mfumo wa Serikali mtandao kutoka taasisi yoyote ya umma ili kutathmini uzingatiaji wa masharti ya Sheria hii.

(2) Tathmini na ukaguzi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, inaweza kufanywa na wakaguzi wa mfumo wa Mamlaka.

(3) Mamlaka, endapo tathmini au ukaguzi utabaini kwamba, taasisi ya umma imekiuka masharti yoyote ya Sheria hii, kanuni, miongozo au taratibu, itaijuulisha taasisi ya umma kwa maandishi, itaeleza:

(a) matokeo ya ripoti ya tathmini na ukaguzi;

(b) hatua zinazohitajika kurekebisha kwa kutofuata masharti; na

(c) muda ambao taasisi ya umma itachukua hatua za kurekebisha.

Upokeaji wa taarifa kwa taasisi za umma.

**41.-**(1) Taasisi ya umma, endapo itaridhia kupokea taarifa yoyote kwa njia ya kielektroniki, itafuata taratibu zilizoainishwa katika Kanuni zinazohusiana na:

(a) namna na muundo ambao taarifa itawasilishwa kwake;

(b) aina au njia ya saini ya kielektroniki inayohitajika, ikiwa ipo;

(c) hatua na taratibu zinazohitajika ili kudhibiti na kuhakikisha uadilifu, usalama na usiri wa taarifa; na

(d) sifa nyengine yoyote kwa taarifa ambayo kwa sasa imeainishwa kwa taarifa zinazolingana katika karatasi.

(2) Endapo sheria inaruhusu taarifa kuwasilishwa au kuhifadhiwa katika mfumo wa kieletroniki, mtu hatohitaji kwamba taarifa inayowasilishwa ipokelewe kwa njia ya kieletroniki na taasisi ya umma tofauti na ilivyoanishwa au inavyotakiwa na hiyo taasisi ya umma.

Utambuzi na Usimamizi wa mtumiaji wa Serikali Mtandao.

**42.** Kwa kuzingatia miongozo itakayotolewa na Mamlaka, taasisi ya umma, kwa madhumuni ya utambuzi wa mtumiaji wa Serikali Mtandao, itahakikisha;

(a) inamthibitisha mtumiaji wa mfumo wa TEHAMA kwa kumpatia utambulisho wa kuweza kutumia mfumo kwa kumthibitisha kulingana na matakwa ya huduma husika;

(b) inamfuatilia kimtandao kuhakikisha matumizi sahihi na kumsitisha kutumia endapo hahitajiki kuendelea na matumizi husika;

(c) inafanya ukaguzi wa kimfumo na ufuatiliaji wa tabia zisizo za kawaida kimtandao; na

(d) inamtaarifu mtumiaji wa mfumo wa TEHAMA kuhusu majukumu yao ya usalama wa TEHAMA.

Uthibitisho wa kupokea nyaraka za kielektroniki.

**43.-**(1) Endapo, katika au kabla ya kutuma nyaraka ya kielektroniki, aliyetuma anabainisha kwa mpokeaji kwamba mawasiliano ya nyaraka hiyo ni ya masharti juu ya upokeaji wa uthibitisho, nyaraka hiyo itachukuliwa kama ni baina ya aliyetuma na mpokeaji.

(2) Endapo kutakuwa hakuna makubaliano baina ya aliyetuma na mpokeaji kuhusu muundo au njia ya uthibitisho, mpokeaji anaweza

kuthibitisha kwa kutumia njia yoyote ya mawasiliano, ya kielektroniki, ya moja kwa moja au vyenginevyo, au kwa tendo lolote ambalo linatosha kubainisha kwa aliyetuma kwamba, nyaraka ya kielektroniki imepokelewa na mpokeaji.

(3) Uthibitisho wa upokeaji uliotolewa na mpokeaji utachukuliwa kama uthibitisho wa msingi kwamba, nyaraka ya kieletronoki imepokelewa na mpokeaji, lakini hakuna chochote katika kifungu kidogo hiki kitakachochukuliwa kumaanisha kwamba nyaraka ya kieletroniki iliyotumwa inalingana na nyaraka ya kieletroniki iliyopokelewa.

(4) Maelezo katika kuthibitisha upokeaji yaliyotolewa na mpokeaji kwamba, nyaraka ya kielektroniki inayohusiana imekidhi masharti ya kitaalamu, ama imekubaliwa baina ya aliyetuma na mpokeaji au imewekwa katika viwango vinavyotumika, itachukuliwa kama uthibitisho wa msingi kwamba masharti hayo yametimizwa.

(5) Isipokuwa kwa kadiri inavyohusiana na utumaji au upokeaji wa nyaraka ya kielektroniki, kifungu hiki hakitaathiri matokeo ya kisheria yanayoweza kutokea ama kutoka katika nyaraka hiyo ya kielektroniki au uthibitishaji wa upokeaji wake.

(6) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, kifungu hiki kitatumika endapo, mpokeaji nyaraka atathibitisha upokeaji wa nyaraka.

Uamuzi wa uhalisia wa ujumbe wa data.

**44.** Taasisi ya umma, kwa madhumuni ya kuamua uhalisia wa ujumbe wa data chini ya Sheria hii, itahakikisha kwamba, usahihi wa taarifa yoyote utatathminiwa kwa kuzingatia iwapo taarifa hiyo imebakia kama ilivyo na haikubadilishwa, isipokuwa kwa nyongeza ya uidhinishaji wowote na mabadiliko yoyote ambayo yanayotokea katika hali ya kawaida ya mawasiliano, uhifadhi na maonyesho.

Uchapishaji wa nyaraka katika Gazeti Rasmi la Serikali la kielektroniki.

**45.** Endapo sheria yoyote inaeleza kwamba waraka wowote uchapishwe katika Gazeti Rasmi, sharti hilo litachukuliwa kuwa limetimizwa ikiwa waraka huo umechapishwa katika Gazeti Rasmi au Gazeti Rasmi la Serikali la kielektroniki.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha na rasilimali za Mamlaka.

**46.** Fedha na rasilimali za Mamlaka zitajumuisha:

(a) fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha zinazopokelewa kutokana na ruzuku, zawadi, misaada, michango au mikopo kama Mamlaka itakavyopokea kutoka kwa mtu au taasisi yoyote;

(c) fedha zinazopokelewa kwa huduma zinazotolewa na Mamlaka;

(d) mapato yanayotokana na uwekezaji utakaofanywa na Mamlaka; na

(e) fedha nyengine zozote zinazoweza kupatikana au kupokelewa kihalali na Mamlaka.

Bajeti.

**47.** Bajeti ya Mamlaka itaandaliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016 na maelekezo mengine yoyote yatakayotolewa na Serikali kila baada ya muda.

Hesabu na ukaguzi.

**48.-**(1) Mamlaka itaweka kumbukumbu za vitabu vya hesabu ya miamala yote na kuhakikisha kwamba fedha zote zilizopokelewa na kulipwa na Mamlaka zinasimamiwa, zinaidhinishwa na kudhibitiwa vizuri dhidi ya mali na madeni yake.

(2) Hesabu za mwaka za Mamlaka zitakaguliwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam.12 ya 2016 na sheria nyengine yoyote za fedha inayohusika.

Uwezo wa kuwekeza.

**49.** Mamlaka itakuwa na uwezo wa kuwekeza fedha zake katika uwekezaji ambao utakuwa na faida, salama na halali kwa mujibu wa sheria husika.

## SEHEMU YA NANE
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu.

**50.-**(1) Mtu ambaye:

(a) kinyume na sheria ametoa au amesambaza data yoyote au kumbukumbu ya kielektroniki iliyopatikana katika utendaji wa kazi;

(b) amepakua vitu visivyoruhusiwa kwa kutumia vifaa au miundombinu ya TEHAMA ya Serikali kama inavyoamuliwa na Mamlaka;

(c) amesambaza au atatoa taarifa au data rasmi kupitia njia isiyoruhusiwa;

(d) amejipatia taarifa au programu kupitia vifaa vya TEHAMA vya Serikali bila ya ruhusa;

(e) kinyume na sheria ameondoa, ameharibu, amebadilisha au ameharibu data yoyote au kumbukumbu ya kielektroniki au miundombinu ya TEHAMA au vifaa vya TEHAMA;

(f) kwa kujua au kwa uzembe ameshindwa kufuata miongozo na viwango vya kiufundi vilivyowekwa kuhusiana na masuala ya usalama ya TEHAMA; au

(g) ameshindwa kuzingatia masharti ya Sheria hii kuhusiana na utekelezaji wa mradi wa TEHAMA,

ametenda kosa na, akipatikana na hatia:

(i) ikiwa ni kosa chini ya aya ya (a), (c), (d) na (f), atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili faini na kifungo; na

(ii) ikiwa ni kosa chini ya aya ya (b), (e) na (g), atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tatu za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Tano za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na isiyozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili faini na kifungo.

(2) Mtumishi wa umma ambaye atakiuka masharti ya Sheria hii, ataadhibiwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011 au sheria nyengine yoyote husika.

Adhabu ya ziada.

**51.** Endapo mtu atatiwa hatiani chini ya Sheria hii, Mahakama inaweza, mbali na adhabu iliyotolewa kwa kosa hilo, kuamuru:

(a) mtu huyo kulipa kwa Mamlaka gharama ya kukarabati uharibifu aliyousababisha; au

(b) kifaa chochote kilichotumika katika kusababisha kosa kwa mtu huyo kutaifishwa au kuharibiwa kwa gharama zake ikiwa kifaa hicho kinamilikiwa na mtu huyo.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI MENGINEYO

Kinga.

**52**. Mjumbe wa Bodi au mfanyakazi wa Mamlaka hatowajibika kwa jambo lolote alilofanya au aliloacha kulifanya ikiwa jambo hilo limefanywa au limeachwa kufanywa kwa nia njema katika kutekeleza kazi au uwezo wa Mamlaka chini ya Sheria hii.

Ubunifu.

**53.-**(1) Kazi yoyote ya TEHAMA iliyoanzishwa, iliyobuniwa au iliyofanywa na Taasisi ya umma itakuwa mali ya Serikali na haitoruhusiwa kutumika kwa faida yoyote ya kibinafsi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtumishi wa umma anayeanzisha, anayebuni au anayefanya ubunifu wowote wa TEHAMA kuhusiana na utoaji wa huduma za umma kwa juhudi zake binafsi anaweza kutunukiwa kwa juhudi zake kama itakavyoamuliwa na Waziri.

Ripoti ya mwaka.

**54. .-**(1) Mamlaka itatayarisha Ripoti ya mwaka na kuiwasilisha kwa Rais ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilika kwa mwaka wa fedha.

(2) Ripoti ya Mwaka iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki itajumuisha shughuli muhimu za Mamlaka kwa mwaka husika, mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika kipindi hicho, pamoja na mipango ya Mamlaka kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Kutofautiana kwa sheria.

**55.** Endapo kutakuwa na mgongano baina ya masharti ya Sheria hii na sheria nyengine yoyote kuhusu masuala yanayohusiana na Serikali mtandao, masharti ya Sheria hii yatatumika.

**56.** Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii. Kanuni.

**57.-**(1) Sheria ya Wakala wa Serikali mtandao Zanzibar, Nam. 12 ya 2019, inafutwa. Kufuta na kubakiza.

(2) Bila ya kuathiri kufutwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa chini ya Sheria iliyofutwa kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, litaendelea na kuchukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI

## MWENENDO WA BODI
**[Chini ya kifungu cha 13]**

**1.** Wajumbe wa Bodi, katika kikao chao cha kwanza, watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti. Makamu Mwenyekiti.

**2.** Isipokuwa mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu. Muda wa wajumbe wa Bodi.

**3.-**(1) Bodi itakutana kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana muda wowote itakapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake. Vikao vya Bodi.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti, ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao cha Bodi na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe watakaokuwepo watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

**4.** Zaidi ya nusu ya wajumbe wa Bodi wataunda akidi katika kikao chochote cha Bodi. Akidi ya vikao.

**5.** Bodi itafanya maamuzi yake kwa makubaliano na endapo hakutakuwa na makubaliano, uamuzi utafanywa kwa kupiga kura na endapo kura zitafungana, Mwenyekiti atakuwa na kura ya maamuzi. Uamuzi wa Bodi.

**6.** Bodi itakuwa na uwezo wa kujipangia utaratibu wake wenyewe kuhusiana na vikao na uendeshaji mzuri wa shughuli zake ikijumuisha kamati za Bodi. Taratibu za mikutano ya Bodi.

**7.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria mijadala yoyote ya vikao vya Bodi kama mtaalamu lakini mtu huyo aliyealikwa hatakuwa na haki ya kupiga kura. Mjumbe mualikwa.

Kumbukumbu za vikao vya Bodi .

**8.** Kumbukumbu za vikao vya Bodi zitathibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata na kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu.

Kamati za Bodi.

**9.-**(1) Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha Kamati kwa ajili ya kutekeleza kazi maalum kama itakavyoona inafaa.

(2) Wajumbe wa Kamati zilizoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, watakuwa miongoni mwa wajumbe wa Bodi au vyenginevyo kama itakavyoamuliwa na Bodi.

Kukasimu kazi .

**10.-**(1) Bodi inaweza, kwa kuzingatia vigezo na masharti kama itakavyoona inafaa, kukasimu baadhi ya majukumu au mamlaka yake kamati ya Bodi.

(2) Endapo Bodi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa miongozo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kazi hizo.

Kubainisha maslahi.

**11.-**(1) Mjumbe wa Bodi ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusika au linalotakiwa kuzingatiwa na Bodi, haraka iwezekanavyo baada kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni wa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji wa maslahi utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha:

(a) hatohudhuria katika majadiliano ya Bodi katika kufanya maamuzi; au

(b) hatomshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya maamuzi.

Kusita kuwa mjumbe.

**12.** Mjumbe atasita kushika nafasi yake iwapo:

(a) amemaliza muda wake;

(b) ameshindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila kueleza sababu za msingi kwa Mwenyekiti;

(c) amejiuzulu au kwa njia yoyote amepoteza sifa yoyote ya ujumbe wa Bodi;

(d) ameshindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu za afya ya kimwili au ya kiakili; au

(e) amefariki.

Posho la wajumbe.

**13.** Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watalipwa posho kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 12 ya 2011.

## MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu ni kufuta Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao, Nam. 12 ya 2019, na kutunga Sheria ya Mamlaka Serikali Mtandao kwa madhumuni ya usimamizi wa masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Utumishi wa Umma Zanzibar.

Mswada huu pia una lengo la kuongeza nguvu za kisheria ili kusimamia na kudhibiti matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma, matumizi ya mifumo mbalimbali katika Serikali, kuweka viwango vya matumizi ya vifaa vya TEHAMA, kuweka utaratibu mzuri wa uanzishwaji na uendelezaji wa mifumo ya kieletroniki, utaratibu wa pamoja wa ununuzi na matumizi ya vifaa vya TEHAMA, uratibu mzuri wa mawasiliano kwa njia ya kielektroniki katika utumishi wa umma, uhifadhi na utumiaji wa taarifa za Serikali kwa njia za kielektroniki na uratibu na uendelezaji wa rasilimali watu ya TEHAMA.

Mswada huu umeundwa na sehemu Tisa;

***Sehemu ya Kwanza:*** inaelezea Masharti ya awali ambayo yanajumuisha na jina fupi na kuanza kutumika, matumizi na ufafanuzi wa baadhi ya maneno yaliyotumika ndani ya Sheria hii.

***Sehemu ya Pili:*** inazungumzia Uanzishwaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar, muhuri na nembo ya Mamlaka. Aidha, kazi na Uwezo wa Mamlaka zimeelezewa katika sehemu hii.

***Sehemu ya tatu:*** inaelezea Uendeshaji na Usimamizi wa Mamlaka ambapo Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka imeaanzishwa ambayo itakuwa ndio chombo kikuu cha usimamizi wa Mamlaka. Sehemu hii pia inaelezea masharti yanayohusiana na kazi na uwezo wa Bodi, uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, sifa na kazi za Mkurugenzi Mkuu, muundo wa Mamlaka na Wafanyakazi wa Mamlaka.

***Sehemu ya Nne:*** inaeleza kuhusu masharti yanayohusiana na Mifumo na huduma za Serikali Mtandao ambapo misingi mikuu ya Serikali Mtandao imeelezewa, pamoja na kumbukumbu, malipo na njia za malipo ya kieletroniki, uhalali wa taarifa za kielektroniki, upatikanaji wa majalada, uimarishaji wa taratibu za kiutawala, masharti yanayohusiana na utoaji wa Data, masharti ya kutoa taarifa kwa maandishi, kubadilishana data, ujazaji wa nyaraka za kielektroniki, saini ya kielekroniki na utoaji wa nyaraka, kizuizi cha matumizi ya data binafsi, kutokutolewa kwa taarifa zilizopewa taasisi za Umma, usalama wa taarifa, ulinzi wa Data, utambulisho na uthibitisho na masharti ya saini ya kielektroniki.

***Sehemu ya tano***: inaelezea masharti yanayohusiana na usimamizi wa huduma za Serikali mtandao ikijumuisha njia ya mawasiliano ya kimtandao, kutunza siri, mifumo ya TEHEMA na manunuzi ya vifaa na programu za TEHAMA.

***Sehemu ya Sita:*** inahusu usalama wa mfumo wa taarifa na miamala ya kielektroniki. Sehemu hii inaelezea kuanzishwa kwa Kituo cha operesheni ya Usalama cha Serikali Mtandao, usalama wa taarifa, ukaguzi wa mifumo ya serikali mtandao, upokeaji wa taarifa kwa taasisi za umma, uthibitisho wa kupokea nyaraka kielektroniki, uwamuzi wa uhalisi wa ujumbe wa data na Uchapishaji wa nyaraka katika Gazeti Rasmi la Serikali la kielektroniki.

***Sehemu ya Saba:*** inazungumzia masharti ya fedha na rasilimali za Mamlaka, bajeti, hesabu na ukaguzi na uwezo wa kuwekeza.

***Sehemu ya Nane:*** inaelezea kuhusu Makosa na Adhabu pamoja na adhabu za ziada.

***Sehemu ya Tisa:*** inaeleza Masharti Mengineyo ikijumuisha na kinga, ubunifu, ripoti ya mwaka, kutofautiana kwa Sheria kisheria, kanuni kufuta Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibari, Nam. 12 ya 2019 na kubakiza.

***Mwisho,*** kuna Jadweli ambalo linaeleza masharti yanayohusiana na mwenendo wa Bodi

**ZANZIBAR**
7 Novemba, 2023

(MHE. HAROUN ALI SULEIMAN)
**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA**

**LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR -2023**